

Christian Faith and Practice in the Friends Church

Friends United Meeting in East Africa

Index

Part 1: Faith

| | |
|-----------------------------|---|
| Trinity | 4 |
| Scripture | 4 |
| Sin and Salvation | 4 |
| Eternal Life | 4 |
| Hell | 5 |
| Prayer | 5 |
| Purpose of the Church | 5 |
| Baptism and Communion | 6 |
| Spiritual Maturity | 6 |
| Spiritual Gifts | 8 |

Part 2: Practice

| | |
|------------------------------|---|
| General Principles | 9 |
| Background | |
| Purpose of Meetings | |
| Church Governance | |
| Speaking in Business Meeting | |
| Consensus | |
| Decisions Recorded | |
| Minutes | |
| Choosing Officers | |
| Approved Authority | |
| Term Limitations | |
| Integrity | |

Imani na Matendo ya Kikristo katika Kanisa la Marafiki

Muungano wa Mkutano wa Marafiki, Afrika Mashariki

Yaliyomo

Sehemu ya Kwanza: Imani

| | |
|---------------------------|---|
| Utatu wa Mungu | 4 |
| Maandiko Matakatifu | 4 |
| Dhambi na Wokovu | 4 |
| Uzima wa Milele | 4 |
| Jehanamu | 5 |
| Maombi | 5 |
| Kusudio la Kanisa | 5 |
| Ubatizo na Ushirika | 6 |
| Ukomavu wa Kiroho | 6 |
| Vipawa vya Kiroho | 8 |

Sehemu ya Pili: Desturi

| | |
|-------------------------------|---|
| Kanuni za Kawaida | 9 |
| Mwanzo | |
| Kusudio la Mikutano | |
| Uongozi wa Kanisa | |
| Kuongea Katika Mikutano Rasmi | |
| Maelewano | |
| Maamuzi Yaliyoafikiwa | |
| Kumbukumbu za Mikutano | |
| Uteuzi wa Viongozi | |
| Uidhinishaji | |
| Muda wa Kuhudumu | |
| Uadilifu | |

| | |
|---|----|
| Village and Monthly Meetings | 11 |
| Village Meeting | |
| Monthly Meeting | |
| Pastor | |
| Meeting for Business | |
| Presiding Clerk duties | |
| Vice Presiding Clerk | |
| Recording Clerk | |
| Financial Affairs | |
| Treasurer | |
| Trustees | |
| Yearly Meeting | 17 |
| Description | |
| Authority | |
| Quarterly Meetings | |
| New Yearly Meetings | 18 |
| Yearly Meeting Operations | 18 |
| Officers | |
| Staff | |
| Appointments | |
| General Superintendent Responsibilities | |
| General Secretary Responsibilities | |
| Annual Sessions..... | 19 |
| Yearly Meeting Structure | 19 |
| General Board | |
| Executive Committee | |
| Nominating Committee | |
| Terms of Appointees | |
| Yearly Meeting Trustees | 21 |
| Responsibilities | |

| | |
|--------------------------------------|----|
| Mikutano ya Kijiji na ya Mwezi | 11 |
| Mkutano wa Kijiji | |
| Mkutano wa Mwezi | |
| Mchungaji | |
| Mkutano Rasmi | |
| Wajibu wa Msimamizi Mkuu | |
| Naibu wa Msimamizi Mkuu | |
| Karani Mwandishi | |
| Shughuli za Kifedha | |
| Mweka Hazina | |
| Wadhamini | |
| Mkutano wa Mwaka | 17 |
| Maelezo | |
| Mamlaka | |
| Mikutano ya Miezi Mitatu | |
| Mikutano Mipya ya Mwaka | 18 |
| Shughuli za Mkutano wa Mwaka | 18 |
| Viongozi | |
| Wafanyi Kazi | |
| Uteuzi | |
| Majukumu ya Mchungaji Mkuu | |
| Majukumu ya Katibu Mkuu | |
| Vikao vya Kila Mwaka..... | 19 |
| Muundo wa Mkutano wa Mwaka | 19 |
| Bodi Kuu | |
| Kamati Kuu | |
| Kamati ya Uteuzi | |
| Muda wa Kuhudumu | |
| Wadhamini wa Mkutano wa Mwaka | 21 |
| Majukumu | |

| | |
|---|----|
| Ethics | |
| Vacancies | |
| Successor Ownership | |
| Yearly Meeting Finances | 22 |
| Treasurer | |
| Finance Committee | |
| Ministers and Pastors | 23 |
| Ministers | |
| Registered Pastors | |
| Unregistered Pastors | |
| Elders/Overseers..... | 24 |
| Term of Appointment | |
| Qualifications | |
| Responsibilities | |
| Role in Church Discipline | |
| Meetings and Confidentiality | |
| Friends United Meeting and Other Affiliations..... | 25 |
| Membership Responsibilities | |
| FUM Board Members | |
| USFWI and Quaker Men | |
| Young Friends | |
| Regional Grouping of Yearly Meetings | |
| Constitutions..... | 27 |
| Writers and Editors | 28 |
| Appendix A: Richmond Declaration of Faith..... | 29 |
| Appendix B: George Fox's Letter to the Governor of Barbados | 46 |

| | |
|---|----|
| Maadili | |
| Nafasi | |
| Urithi | |
| Fedha za Mkutano wa Mwaka | 22 |
| Mweka Hazina | |
| Kamati ya Fedha | |
| Watumishi na Wachungaji | 23 |
| Watumishi | |
| Wachungaji Waliosajiliwa | |
| Wachungaji Wasiosajiliwa | |
| Wazee wa Kanisa..... | 24 |
| Muda wa Kuhudumu | |
| Masharti | |
| Majukumu | |
| Majukumu ya Wazee wa Kanisa kuhusu Nidhamu Kanisani | |
| Mikutano na Faragha | |
| Muungano wa Mkutano wa Marafiki na Mashirika Mengine..... | 25 |
| Majukumu ya Wanachama | |
| Wanachama wa bodi ya Muungano wa Mkutano wa Marafiki | |
| Muungano wa Wanawake wa Marafiki (USFW) na Muungano wa Wanaume wa Marafiki (Quaker Men) | |
| Mkutano wa Vijana wa Marafiki | |
| Vikundi vya Kimaeneo vya Mikutano ya Mwaka | |
| Katiba | 27 |
| Waandishi na Wahariri..... | 28 |
| Nyongeza A: Uamuzi wa Imani wa Richmond..... | 29 |
| Nyongeza B: Barua ya George Fox kwa Mtawala wa Babadosi | 46 |

Part I: Faith

1) Trinity

- a) Friends are in unity with all Christians in our belief in: God the Creator, infinite in love, wisdom and power, the source and sustainer of all life;
- b) God's divine Son, Jesus Christ, whose life, death and resurrection reveal the nature and reality of God;
- c) The gift of the Holy Spirit, the ever-present Comforter Who is God's seal upon us so that we may know we belong to God.

2) Scripture

Friends accept the Holy Bible, consisting of the Old and New Testaments as:

- a) Inspired by God
- b) The written Word of God
 - i) The Bible, read through the eyes of prayer, tells us about the nature and promises of God; the work and message of our Saviour, Jesus Christ; and the right conducts of life as individuals and life in the Church.
 - ii) No doctrine or prophecy, which is in conflict with the message of the Bible, can be accepted among Friends.

3) Sin and Salvation

Friends believe in the reality of sin and the reality of salvation. With our weaknesses and limitations, we humans often disobey God: we disobey the Commandments which God gave us through Moses for our own good; we insult each other despite the plain warnings of Scripture; we allow false idols to divert us from God; we separate ourselves from God by pursuing power, money, pleasure or vengeance. Sin can infect whole societies, resulting in spiritual, social and economic oppression.

4) Eternal Life

God sent Jesus Christ to save us from the power of sin and bring us back into full fellowship with God. God does not want anyone to perish unsaved

Sehemu Ya Kwanza: Imani

1) Utatu wa Mungu

- a) Marafiki wana umoja na wakristo wote kwa imani kuwa: Mungu Muumba, mwingi wa upendo, hekima na uwezo, chanzo na mhifadhi wa uhai wote;
- b) Mwana Mtakatifu wa Mungu, Yesu Kristo, ambaye uhai wake, kifo na ufufuo wake unaonyesha uja na uhalisi wa Mungu;
- c) Kipawa cha Roho Mtakatifu, mfariji wa daima na ambaye ni ishara ya Mungu kwetu ili tujue kuwa sisi ni sehemu yake Mungu.

2) Maandiko Matakatifu

Marafiki wamekubali Biblia Takatifu, kuanzia Agano la Kale hadi Agano Jipya kama:

- a) Yaliandikwa kwa uvuvizi wa Mungu
- b) Neno la Mungu lililoandikwa
 - i) Biblia, ikisomwa kupitia kwa maombi, inatuelezea kuhusu asili na ahadi za Mungu; kazi na ujumbe wa Mwokozi wetu, Yesu Kristo; na mienendo sahihi ya maisha ya wanadamu ya kibinafsi na ya kikanisa.
 - ii) Hakuna kanuni wala unabii, ambao unahitilafiana na ujumbe wa Biblia, unaweza kukubalika miongoni mwa Marafiki.

3) Dhambi na Wokovu

Marafiki wanaamini katika uhakika wa dhambi na wa wokovu. Kwa undhaifu wetu, sisi wanadamu aghalabu tunamuasi Mungu: tunaasi kanuni ambazo Mungu alitupatia kupitia kwa Musa kwa manufaa yetu; tunatusiana ijapokuwa tunafahamu dhahiri onyo la maandiko; tunaruhusu sanamu za uongo kutupotosha kutoka kwa Mungu; tunajitenga kutoka kwa Mungu na kukimbilia mamlaka, pesa, anasa ama kisasi. Dhambi inaathiri jamii nzima, na matokeo huwa ni kutaabika kwa hali ya kiroho, kijamii na kiuchumi.

4) Uzima wa Milele

Mungu alimtuma Yesu Kristo kutuokoa kutoka kwa mamlaka ya dhambi na kutuweka katika ushirika kamili na Mungu. Mungu hataki kumwona

and has given each of us the capacity and opportunity to hear the invitation of Jesus to be restored to God; to live with God eternally. When we confess that we have sinned and repent and ask Jesus to come into our lives, to be our Lord and Saviour, He can heal the wounds of sin and break the power of sin over us.

5) Hell

Those who remain obstinate in sin and persist in ignoring the invitation of Jesus to be forgiven and saved are in grave danger of eternal separation from God. This state of eternal separation from God is known as hell.

Friends believe in the reality of evil. There is a power in the world, which wants to enslave us and turn us from God's purposes; we call that evil Satan. Satan is called the "father of lies" and the "author of confusion" because this power tries to deceive us and keep us from seeing God's light. When we fall into sin, we are in great danger of cooperating with evil. God is more powerful than Satan. Through confession and repentance of sin, God is able to overcome sin in our lives.

6) Prayer

Friends believe in the central importance of prayer. To pray is communicating with God – both listening and speaking. Prayer is turning to God either in words or in our thoughts and attitudes, in order to enjoy God's presence, to listen to God, to love and praise God, to bring our sins to God and ask for forgiveness, to ask God's help for ourselves and for others, and to thank God.

7) Purpose of the Church

Friends are a church, a part of the larger Christian church, which is the Body of Christ in the world. The purposes of the church are to gather at the feet of the Saviour and learn from him, to praise and worship him, to support each other as we learn to be more faithful followers of Jesus, and to express the good news of Jesus Christ in each of our communities and to the rest of the world, so that others may be saved. More specific information about the organisation and work of the church is given in Part 2, Friends' Practices.

mwanadamu yeyote akiangamia bila kuokoka na ametupatia kila mmoja wetu uwezo na nafasi kuitikia mwito wa Yesu wa kurejeshwa kwa Mungu; kwa kuishi naye milele. Tunapokiri kuwa tumekosa na kutubu na kumuomba Yesu kuingia ndani ya maisha yetu, kama Bwana na Mwokozi, kwa kuponya majeraha ya dhambi, kwa kuharibu uwezo wa dhambi juu yetu.

5) Jehanamu

Wale wanaokaidi kutoka kwa dhambi kwa kupuuza mwito wa Yesu wa kusamehewa na kuokolewa, wako katika hatari kubwa ya kutengwa milele kutoka kwa Mungu. Hali hii ya kutengwa milele kutoka kwa Mungu ni jehanamu.

Marafiki wanaamini katika uhalisi wa uovu. Kuna mamlaka katika ulimwengu yanayotuweka watumwa na kutugeza kutoka kwa maksudio ya Mungu; tunamuita huyo mwovu Shetani. Shetani anaitwa "baba wa uongo" na "mwasisi wa suitafahamu" kwa sababu haya mamlaka hujaribu kutudanganya na kutuzuia tusiione nuru ya Mungu. Tunapotenda dhambi, tuko katika hatari kubwa ya kushirikiana na uovu. Mungu ana mamlaka kuliko Shetani. Kwa kukiri na kutubu dhambi, Mungu anaweza kutushindia dhambi katika maisha yetu.

6) Maombi

Marafiki wanaamini kwa umuhimu wa Maombi. Kuomba ni kuwasiliana na Mungu – kwa kusikiliza na kuongea. Maombi ni kuwasiliana na Mungu labda kupitia kwa maneno, fikra au mielekeo ili kuufurahia uwepo wa Mungu, kumsikiliza, kumpenda na kumsifu Mungu, kuziweka dhambi zetu kwa Mungu na kuomba msamaha, kuuliza usaidizi wa Mungu kwetu na kwa wengine na kumshukuru.

7) Kusudio la Kanisa

Marafiki ni kanisa, ambalo ni sehemu kubwa ya wakristo, ambao ni Mwili wa Kristo ulimwenguni. Malengo ya kanisa ni kukusanyika chini ya miguu ya Mwokozi na kujifunza kutoka kwake, kumsifu na kumuabudu, kusaidiana wenyewe kwa wenyewe tunapojifunza kuwa wafuasi waaminifu sana wa Yesu kwa kutangaza habari njema yake kwa kila mojawapo ya jamii zetu na kwa wengine wote duniani, ndiposa waweze kuokolewa. Taarifa kamili kuhusu utaratibu na kazi ya kanisa imetolewa katika sehemu ya pili ya kitabu hiki.

8) Baptism and Communion

Friends believe that there is one Lord, one faith and one true baptism that unites the new believer with the whole Body of Christ (Ephesians 4:4-5, 1 Corinthians 12:13). This baptism is a spiritual experience of dying to self and being reborn by the power of the Resurrection of Christ (1 Peter 3:21 and Romans 6:4). Without this experience, a water baptism or other ceremony does not suffice, and with this experience, a ceremonial baptism is not necessary.

Similarly, our communion with Jesus Christ cannot be simply an outward reenactment of a literal eating of His body and drinking of His blood, but a full remembrance of his sacrifice through prayer and waiting upon the Holy Spirit. For a fuller treatment of baptism and communion, see Appendix A, *The Richmond Declaration of Faith*.

9) Spiritual maturity

When we accept Jesus Christ as our Saviour and allow him to be Lord of our life, we become his disciples – his students. Jesus teaches us how to live. Instead of following self-centered ways of sin, as we did before, we walk in a new direction, following Jesus. We can no longer accept values set by society. All spiritual, moral and ethical values must be set by Scriptural standards. It is for this reason that the Friends church teaches testimonies to:

- a) Peace and nonviolence – When the world tells us to hate our enemies, we follow Jesus' command to love them. When the world seeks violence, we seek non-violent resolution to conflict. We remain the harmless and innocent children of God, denying anyone the right to put weapons into our hands once we have dedicated those hands to the service of God. Our fight is not against other people, but against the forces of evil. (Ephesians 6:12)
- b) Simplicity – Friends practice moderation in all things. Jesus teaches that we cannot serve both God and money and that anxiety will not add anything to our lives. Material possessions and money, higher education or careers in government or management do NOT make persons more important than those with less. We are equal in the

8) Ubatizo na Ushirika

Marafiki wanaamini kuwa kuna Bwana mmoja, imani moja na ubatizo mmoja wa kweli unao unganisha muumini mpya na Mwili wote wa Kristo (Waefeso 4:4-5; 1 Wakorintho 12:13). Ubatizo huu ni tukio la kiroho la kuzaliwa kwa mwanadamu na kufufuliwa kwa uwezo wa ufufuo wa Kristo (1 Petro 3:21 na Warumi 6:4). Bila tukio hili, ubatizo wa maji wala sherehe zingine hazawezi kuwa na manufaa yoyote.

Vivyo hivyo, ushirika wetu na Yesu Kristo hauwezi kuwa tu wa kula mwili na kunywa damu yake, bali ni ukumbusho kamili wa kupitia kwa maombi na Roho Mtakatifu. Kwa maelezo kamili ya ubatizo na ushirika, tazama Nyongeza A, *Uamuzi wa Imani wa Richmond*.

9) Ukomavu wa Kiroho

Tunapomkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wetu na kumruhusu kuwa Bwana wa maisha yetu, tunakuwa wafuasi wake – wanafunzi wake. Yesu hutufundisha jinsi ya kuishi. Badala ya kufuata mienendo ya dhambi ya kujifikiria wenyewe, kama tulivyofanya awali, tumepata mwelekeo mapya wa kumfuata Yesu. Hatuwezi kukubali maadili yaliyowekwa na jamii. Maadili yote ya kiroho na uadilifu lazima yawekwe kulingana na kanuni za maandiko matakatifu. Ni kwa sababu hii, ndipo Kanisa la Marafiki hufundisha ushuhuda kuhusu:

- a) Amani bila vurugu – Ulimwengu unapotwambia kuwa tuwachukie maadui wetu, sisi tunafuata agizo la Yesu la kuwapenda walimwengu. Wanapofanya vurugu, nasi tunafuata njia za amani za kutatua mizozo. Sisi ni wanadamu wazuri mbele ya Mungu, ambao hawataki kutumia silaha kwa mikono iliyowekwa wakfu kwa utumishi wa Mungu. Vita vyetu si dhidi ya watu wengine, bali ni dhidi ya mamlaka ya uovu. (Waefeso 6:12)
- b) Maisha kiasi – Marafiki wana mazoea ya kiasi kwa vitu vyote. Yesu hutufundisha kuwa hatuwezi kumtumikia Mungu pamoja na pesa. Kwani hili halitaongeza chochote kwa maisha yetu. Vitu tunavyomiliki kama pesa na mali, elimu ya juu na uongozi serikalini haviwezi kufanya wanadamu kuwa wa maana kuliko wale ambao

eyes of God. Jesus' teaching is about attitude toward possessions and wealth. It is not sinful to earn money honestly. It is sinful to use that money to mistreat or take advantage of others.

- c) Honesty – God says: Thou shalt not steal and thou shalt not bear false witness. Friends do not steal, accept bribes, misuse the money or assets of others. A Friend tells the truth at all times (Matthew 5:37).
- d) Equality – Friends believe that all people are made in God's image and are equal in God's sight. No race, tribe or language is superior. One sex is not superior over the other. (Galatians 3:28) God's gifts of ministry are bestowed on whomever God desires, regardless of race, sex, physical disability or social status.
- e) Humility – No Friend expects or is granted special treatment because of position, education, or wealth.
- f) Marriage and Sexual Ethics – Friends define marriage as a Godly union of one man and one woman. Sexual intimacy is reserved for the context of marriage. When polygamy is part of the culture, new believers in a polygamous marriage are not expected to break their existing bonds, but to enter no further marriages (Mark 10:7-9). Leaders are to be chosen from among those who are in a monogamous marriage (1 Timothy 3:1-13). Friends believe that marriage is a lifetime commitment made before God. Divorce would occur only in cases of extreme problems such as abuse.
- g) Sanctity of Life – Friends affirm the sanctity of life and oppose abortion as a method of birth control and oppose euthanasia.
- h) Cultural Conflicts – The path to spiritual maturity leads us to change cultural customs and traditions that are in conflict with Scripture. Many cultural customs and traditions are valuable and in union with Scripture. Others must be challenged. This was true for the early Christians, for the first generation of Friends in England, for Friends

hawana au wana vichache. Sisi sote ni sawa mbele ya Mungu. Mafundisho ya Yesu juu ya umilikaji wa mali ni kwamba si dhambi kupata pesa kwa njia halali. Ni dhambi kutumia zile pesa kwa kuwatendea maovu au kuwadanganya wengine.

- c) Uaminifu – Mungu anasema: Usiibe na usishuhudie uongo. Marafiki hawaibi, hawapokei rushwa, hawaharibu pesa wala mali ya wengine. Rafiki husema ukweli wakati wote (Mathayo 5:37).
- d) Usawa – Marafiki wanaamini kuwa wanadamu wote wameumbwa kwa mfano wake Mungu na wako sawa mbele ya Mungu. Hapana taifa, kabila, wala lugha iliyo bora kuliko nyingine. Hakuna jinsia iliyo bora kuliko nyingine. (Wagalatia 2:28) Vipawa vya Mungu vya kumhudumia hupatiwa wale Mungu amechagua, bila kujali taifa, jinsia, asili, ulemavu, au hali ya kijamii.
- e) Unyenyekevu – Hakuna Rafiki ambaye hutarajia kutendewa bora kwa sababu ya cheo, masomo au mali.
- f) Ndoa na maadili ya kingono – Marafiki hubainisha ndoa kuwa muungano wa Mungu wa mume mmoja na mke mmoja. Kujua kimwili ni katika ndoa. Ingawaje tamaduni zinaruhusu ndoa za wake wawili au zaidi waumini wapya katika ndoa hizo hawatarajiwi kuzivunja, wala kuingia katika ndoa zingine (Marko 10:7-9). Yafaa viongozi kuchaguliwa kutoka miongoni mwa wale walio katika ndoa ya mume mmoja na mke mmoja (1 Timotheo 3:1-13). Marafiki wanaamini kuwa ndoa ni ahadi ya maisha iliyofanywa mbele ya Mungu. Talaka itakukubalika tu kama kuna shida kama vile dhuluma.
- g) Umuhimu wa Uhai – Marafiki huthibitisha umuhimu wa maisha na hupinga kuavya kwa mimba kama njia ya kupanga uzazi na hupinga mauaji ya huruma.
- h) Vizuizi vya kitamaduni – ukomavu wa kiroho hutuelekeza kuzibadilisha mila na desturi za tamaduni zinazohitilafiana na maandiko ya Biblia. Desturi na mila nyingi za kitamaduni ni muhimu na zimeambatana na maandiko ya Biblia. Zingine lazima zitupilwe mbali. Ilikuwa hivi kwa wakristo wa kale, kizazi cha kwanza cha

confronting slavery in the USA, and for African Friends today. Careful study and prayer allows Friends to discover God's Truth in all matters.

- i) Christian Life – It is not easy to live a Christian life, constantly rejecting temptation of society's standards in favour of God's standards. For this reason, we need the support and encouragement of the church, and of each other. We need to pray often for God's help to resist sin and oppose the work of Satan, and for God's strength to carry the news of God's victory over all forms of oppression to the entire world.

10) Spiritual Gifts

Friends believe in the gifts of the Spirit as taught by Paul in 1 Corinthians 12 and Ephesians 4. We believe that the gifts listed by Paul and in evidence elsewhere in the New Testament record are distributed according to God's plan among all Christians – old and young, male and female, among those who are illiterate and those of advanced education or physical disability. Spiritual gifts are abilities or capacities which are intended by God to help build up the church – to teach, lead, inspire, pastor, heal, assist, administer, comfort, correct, pray for others. Our spiritual leaders should be chosen by our churches based on evidence that they have the spiritual gifts appropriate for their office.

Spiritual gifts, when used under the guidance and leadership of the Holy Spirit, are to be respected by others.

Marafiki kule Uingereza, kwa Marafiki waliokabilia na utumwa kule Marekani, na kwa Marafiki wa Kiafrika leo. Maombi na uchunguzi wa kina una wapa Marafiki ukweli wa Mungu kuhusu mambo yote.

- i) Maisha ya Ukristo – Si rahisi kuishi maisha ya ukristo, kwa sababu kila mara ni kukataa majaribio ya kijamii kwa ajili ya Mungu. Kwa hivyo, tunahitaji kuungwa mkono na kutiwa moyo na kanisa. Tunahitaji kuomba msaada wa Mungu kila mara ili tuepukane na dhambi na kukataa nguvu za Shetani, ili kueneza habari za ushindi wa Mungu dhidi ya maovu ya aina yote duniani.

10) Vipawa vya Kiroho

Marafiki wanaamini katika vipawa vya Kiroho kama anavyofundisha na Paulo katika 1 Wakorintho 12 na Waefeso 4. Tunaamini kuwa vipawa vilivyotajwa na Paulo na hata kupitia kwa ushahidi kwingineko katika agano jipya, vimegawanywa kwa mapenzi ya Mungu kwa wakristo wote – wakongwe kwa vijana, wanaume kwa wanawake, wasomi na wasio soma au walemavu. Vipawa vya Kiroho ni uwezo ambao Mungu amekusudia uwezeshe kujenga kanisa – kwa kufundisha, kuongoza, kuwezesha, kuchunga, kuponya, kusimamia, kufaraji, kukosoa, kuombea wengine. Viongozi wetu wa kiroho wanafaa kuchaguliwa na makanisa yetu kulingana na ushahidi kuwa wana vipawa vya kiroho vifaavyo kwa huduma zao.

Vipawa vya kiroho vinapaswa kuheshimiwa na wengine vinapotumiwa chini ya mwongozo na Usimamizi wa roho mtakatifu.

Part 2: Practice

1) General Principles

- a) Background. The Religious Society of Friends Church (Quakers) began out of a reform movement within the larger Christian church and does not seek to depart from any of the valid principles and biblical foundation of the Christian church. Early Friends wished to reject the formal church practices that had grown up in the church since New Testament times and sought to return to the power and simplicity of the New Testament church.
- b) Meetings. Friends distinguish three purposes for meetings:
 - i) meetings for worship whose purpose is to introduce people to the salvation through Jesus Christ,
 - ii) meetings for worship where the believers and interested members of the public gather regularly to worship God, and
 - iii) the meeting for business, sometimes called the meeting for church governance. Meetings for business (church governance) should be distinguished from and held at separate occasions from meetings for worship.
- c) Church Governance. In all meetings for church governance, Friends hold the meeting in a spirit of prayer and worship. Friends give unhurried consideration to all proposals and opinions. All members have equal rights and privileges in attendance and participation in decision-making at meetings for church governance.
- d) Speaking at Business Meeting. When speaking in a meeting for church governance, Friends express their sense of what God intends for the congregation, not personal opinion or for personal benefit. Friends who wish to speak stand or indicate to the presiding clerk that they wish to be heard. They do not begin to speak until the presiding clerk gives permission.
- e) Consensus. The concerns and doubts of a sincere minority must be carefully considered before a decision is made. The goal is to reach substantial unity. It may be that some Friends will not be in favor,

Sehemu ya Pili: Desturi

1) Kanuni Jumuishi

- a) Mwanzo. Jamii ya Kanisa la Marafiki (Wakweka) ilianzishwa kutokana na mabadiliko ndani ya kanisa la kikristo na haitarajii kuacha kanuni zozote na msingi wa kibiblia wa kanisa la kikristo. Marafiki wa kale walitamani kutupilia mbali desturi za kanisa, ambazo zilikuwepo tangu wakati wa agano jipya na kurudia ule uwezo na wastani wa kanisa la agano jipya.
- b) Mikutano. Marafiki wanatofautisha sababu tatu za mikutano:
 - i) mikutano ya ibada ambayo nia yake ni kuwaleta watu kwa wokovu kupitia kwa Yesu Kristo,
 - ii) mikutano ya ibada ambayo waumini na watu wengine hukusanyinka mara kwa mara kumuabudu Mungu, na
 - iii) mikutano rasmi, au mikutano ya uongozi wa kanisa. Mikutano rasmi inafaa itofautishwe na ile ya ibada.
- c) Uongozi wa Kanisa. Katika mikutano yote ya uongozi wa kanisa, Marafiki hufanya mkutano kwa hali ya maombi na ibada. Marafiki huafikia maamuzi baada ya maoni ya waliohudhuria kusikizwa na kuzingatiwa kwani wote wana haki na nafasi sawa.
- d) Kuongea katika Mkutano Rasmi. Wakati wa kuzungumza kwenye mkutano wa uongozi wa kanisa, Marafiki husema wazi yale makusudio ya Mungu kwa kanisa na wala siyo maoni ya kibinafsi au ya kujinufaisha. Marafiki wanaotaka kuongea husimama, huihua mikono au hata kutoa ishara kwa msimamizi mkuu ili waongee.
- e) Maafikiano. Tashwishi na wasiwasi ya wachache wenye nia njema, lazima ifikiriwe kwa makini kabla uamuzi kufanywa. Madhumuni ni kufikia umoja wa kweli. Inaweza kuwa Marafiki wengine

but the decision may nevertheless be adopted. When there is much difference of opinion within the congregation, the clerk should postpone a decision to a subsequent meeting to allow more time for prayer and research.

- f) Decisions Recorded. It is the responsibility of the presiding clerk to determine that a decision agreeable to those in attendance has been reached. Decisions are recorded in writing as a minute.
- g) Minutes. Minutes of all Friends business meetings are to be made available to any member who requests them. Recording clerks should take care to ensure that minutes are safely preserved.
- h) Appointing Leaders. Officers, elders, overseers, and committee members are chosen on the basis of their spiritual gifts and general spiritual maturity. Friends do not make distinctions based on age, sex, educational credentials, work or business background, ethnic or tribal background or social class.
- i) Approved Authority. No officer or group within a meeting has any degree of arbitrary or final authority. All decisions affecting personnel, receiving or spending of funds, and the buying, selling or hiring of property, must be authorised by a written minute of the appropriate group. Among Friends, these activities are not carried out solely by an individual or small group acting apart from such authorisation.
- j) Term Limitations. Friends seek a fair distribution of leadership opportunities. Appointments for service among Friends are for one, two or three years and may be renewed. Such appointments, including reappointments, are limited to a maximum of six years, except for Trustees, who may serve a maximum of twelve years. After term limit expiration, a one-year minimum separation is required before possible reappointment. Friends ensure that a range of ages and both sexes are included in appointments. An officer should hold only one position at a time.

hawatakubaliana, lakini uamuzi unaweza kuafikiwa. Ikiwa kuna tofauti sana za maoni, msimamizi mkuu anaweza kuhairisha mkutano hadi wakati mwingine ili kuwapa washirika muda wa kuwa na maombi na kufanya utafiti.

- f) Maamuzi Yaliyoandikwa. Ni jukumu la msimamizi mkuu kuhakikisha kwamba uamuzi unaokubalika na wale waliohudhuria umefikiwa. Maamuzi huandikwa kama kumbukumbu.
- g) Kumbukumbu za mikutano. Kumbukumbu za mikutano rasmi yote ya Marafiki, huwekwa wazi kwa yeyote anayetaka kuzisoma. Makarani waandishi lazima wahakikishe kumbukumbu zote zimehifadhiwa vizuri.
- h) Kuteua Viongozi. Viongozi, wazee, wasimamizi na wanakamati huteuliwa kwa misingi ya vipawa vyao vya kiroho na ukomavu wao wa kiroho. Marafiki hawabagui kwa misingi ya umri, asili, viwango vya masomo, kazi au ujuzi wa kibiashara, taifa, kabila wala tabaka.
- i) Mamlaka Yaliyoidhinishwa. Hakuna kiongozi au kikundi katika mkutano ambacho kina uwezo wa kutoa uamuzi wa mwisho. Uamuzi wote unaohusu wafanyikazi, fedha, na ununuzi au uuzaji wa mali, lazima uidhinishwe na kumbukumbu za kikundi husika. Miongoni mwa Marafiki, shughuli hizi hazifanywi na mtu mmoja tu au kikundi kidogo bila idhini.
- j) Muda wa Kuhudumu. Marafiki huzingatia mgao sawa wa nafasi za uongozi. Uteuzi wa kazi miongoni mwa Marafiki huwa wa mwaka mmoja, miwili au mitatu na unaweza kuongezwa upya. Uteuzi kama huo, pamoja na kuongezea muda, huwa wa miaka sita, isipokuwa kwa wadhamini, ambao wanaweza kutumika hadi miaka kumi na mbili. Baada ya mwisho wa muda wa kuhudumu kumalizika, kuna kipindi cha mwaka mmoja kabla ya uteuzi tena. Marafiki huhakikisha kwamba uteuzi unahusisha jinsia na umri wote. Kila kiongozi huwa na wajibu mmoja kwa wakati mmoja.

- k) Integrity. To avoid temptation and misunderstandings, Friends are extremely careful in their observance of the principles of good business practice, including the procedures listed below in the sections involving treasurers.

2) Village and monthly meetings

- a) The village meeting is the basic unit of Friends organization at the local level. Friends worship every Sunday within their local village meeting and participate in the worship and governance processes of the monthly meeting of which their village meeting is a part. The village meeting:
- i) meets every Sunday for meetings of worship,
 - ii) has a pastor who plans, organizes and conducts meetings for worship,
 - iii) receives new members, guides and counsels them for membership at all levels,
 - iv) keeps records which are normally made known to the monthly meeting, quarterly meeting and finally the yearly meeting,
 - v) is represented at nominating committees of the yearly meeting,
 - vi) has its own finance committee,
 - vii) recommends to the monthly meeting names of members to be disciplined for expressions or conduct inconsistent with Christian discipleship or with this Faith and Practice. Upon consideration of such recommendations, the monthly meeting may:
 - a. work to offer a process for confession, repentance and reconciliation;
 - b. impose a suspension of membership or of leadership responsibilities for a suitable period of restoration;
 - c. remove the member's name from the membership lists.

- k) Uadilifu. Ili kuepukana na kutoelewana, Marafiki huwa waangalifu kwa kuzingatia kanuni nzuri za utendaji kazi, zikiwemo taratibu zilizonakiliwa katika sehemu ya wawekahazina.

2) Mikutano ya kijiji na ya mwezi

- a) Mkutano wa kijiji ndio msingi wa kwanza wa utaratibu wa Marafiki mashinani. Marafiki wanaabudu kila Jumapili katika mkutano wao wa kijiji na hushiriki katika ibada na michakato ya uongozi wa mkutano wa mwezi, ukiwemo wa kijiji. Mkutano wa kijiji:
- i) huwa kila Jumapili kwa mikutano ya ibada,
 - ii) una mchungaji anayeratibu mikutano ya ibada,
 - iii) hupokea washiriki wapya, huwaongoza na kuwashauri kwa kuwashirikisha katika viwango vyote,
 - iv) huweka kumbukumbu ambazo, kwa kawaida husomwa kwa mkutano wa mwezi na wa miezi mitatu na wa mwisho wa mwaka,
 - v) huwakilishwa katika kamati za uteuzi za mkutano wa mwaka,
 - vi) una kamati ya fedha,
 - vii) hupendekeza kwa mkutano wa mwezi majina ya waumini ambao wanafaa kuadhibiwa kwa sababu ya tabia au mienendo isioambatana na ufuasi wa kikristo au imani na matendo. Baada ya kuchunguza mapendekezo hayo, mkutano wa mwezi unaweza:
 - a. kutoa nafasi ya kukiri, kutubu na maridhiano;
 - b. kuamuru kuondolewa kwa muda kwa uanachama au kwa majukumu ya uongozi kwa muda unaofaa;
 - c. Kutoa jina la mwanachama kutoka kwa orodha ya wanachama wengine.

- viii) reaches out to those who are outside the meeting, and involving other members in outreach,
 - ix) provides care of widows and orphans.
- b) The words “monthly meeting” refer to the congregation as well as to the actual gatherings for the transaction of church business, which usually occur monthly. As the governing body, the monthly meeting:
- i) holds the memberships of Friends, receives new members,
 - ii) disciplines members for good cause (see section vii under village meetings),
 - iii) terminates memberships of those who persist in unrepentant disunity with the church,
 - iv) records births and deaths,
 - v) conducts marriages and burials,
 - vi) oversees the finances of the monthly meeting (see below),
 - vii) appoints representatives to the quarterly, regional and yearly meetings.
- viii) It may own property.
- ix) The monthly meeting may be served by one or more pastors, a presiding clerk, a treasurer and other appointed committee members as needed. These offices and functions are described below. A monthly meeting should approve financial budgets made by village meetings.
- c) The pastor is employed by and accountable to the monthly meeting, and is responsible for:
- i) planning, leading and coordinating the public worship of the church,
 - ii) involving other members as participants in worship leadership,
 - iii) providing pastoral care and counseling,
 - iv) conducting marriages and funerals,
 - v) visiting those who are sick,

- viii) kuwafikia wale ambao si waumini na kuwahusisha wengine kuwafikia,
 - ix) kutoa usaidizi kwa wajane na mayatima.
- b) Maneno “mkutano wa mwezi” yana maana ya mkusanyiko wa waumini na pia humaanisha mikusanyiko mingine ya shughuli rasmi ambazo kwa kawaida hufanyika kila mwezi. Kama halmashauri simamizi, mkutano wa mwezi:
- i) ni uanachama wa marafiki na hupokea waumini wapya,
 - ii) huadhibu waumini kwa nia njema (Tazama sehemu ya vii chini ya mkutano wa kijiji),
 - iii) husimamisha uanachama wa wale ambao huendeleza migawanyiko kanisani bila kutubu,
 - iv) husajili kuzaliwa na vifo,
 - v) huendesha ndoa na mazishi,
 - vi) husimamia fedha za mkutano wa mwezi (tazama chini),
 - vii) huteua wakilishi kwa mikutano ya miezi mitatu, eneo na ya mwaka.
- viii) Unaweza kumiliki mali.
- ix) Mkutano wa mwezi unaweza kuhudumiwa na mchungaji mmoja au zaidi, msimamizi mkuu, mweka hazina na wanakamati wateuliwa wengine kama inavyohitajika. Hizi nyadhifa na majukumu yameelezewa hapo chini. Mkutano wa mwezi huidhinisha bajeti za mikutano ya kijiji.
- c) Mchungaji ameajiriwa na anawajibika kwa mkutano wa mwezi kwa:
- i) kuratibu na kuongoza ibada kanisani,
 - ii) kuwashirikisha waumini katika uongozi wa ibada,
 - iii) kutoa nasaha ya kiroho na ushauri,
 - iv) kusimamia ibada za ndoa na mazishi,
 - v) kuwatembelea wagonjwa,

- vi) providing instruction in Christian faith and discipleship,
 - vii) general pastoral administration,
 - viii) reaching out to those who are outside the meeting, and involving other members in outreach,
 - ix) provide care of widows and orphans.
- d) The meeting for business is served by a presiding clerk and an assistant presiding clerk. The presiding clerk opens the meeting for business (also known as the meeting for church governance), at which all members of the monthly meeting are expected to attend. Meetings for business take place at a separate time from meetings for worship, at a time convenient for gathering Friends who may worship at separate locations.
- e) The purpose of the meeting for business is to seek God's will for the business affairs and arrangements of the monthly meeting and its constituent village meetings. Such business decisions may include:
- i) the reception, disciplining or removal of members,
 - ii) the purchase, sale or construction of property,
 - iii) the establishing or closing of constituent meetings for worship,
 - iv) the time and place of meetings for worship,
 - v) consideration of reports from committees, officers, treasurer, Sunday school classes, men's and women's and youth groups,
 - vi) the appointment of pastors and officers,
 - vii) the appointment of women and men to represent the monthly meeting at superior bodies such as quarterly, regional and yearly meeting,
 - viii) the recommendation of men and women who have shown evidence of gifts in public ministry for possible recording by yearly meeting.
- f) The presiding clerk:
- i) opens the meeting for business with prayer,

- vi) kutoa mafunzo ya imani ya kikristo na kuwakuza wanafunzi,
 - vii) usimamizi jumuishi wa uchungaji,
 - viii) kuwafikia wale walio nje ya mkutano, na kuwashirikisha wanachama wengine katika uenezaji wa injili,
 - ix) kuwahudumia wajane na mayatima.
- d) Mkutano rasmi unaongozwa na msimamizi mkuu na naibu wake. Msimamizi mkuu hufungua mkutano (pia huitwa mkutano wa usimamizi mkuu wa kanisa), ambao wanachama wote wa mkutano wa mwezi huhudhuria. Mikutano rasmi hufanyika kwa wakati tofauti na mikutano ya ibada, ili kuwapa nafasi wale wanaotaka kuabudu katika sehamu zingine.
- e) Madhumuni ya mikutano rasmi ni kupanga shughuli rasmi za mkutano wa mwezi na ile ya vijiji husika kwa uwezo wa Mungu. Maamuzi kama haya ya shughuli rasmi yanaweza kujumuisha:
- i) kuwapokea, kuwaadhibu ama kuondoa wanachama,
 - ii) ununuzi, uuzaji ama ujenzi wa mali,
 - iii) kuanzisha ama kufungwa kwa mikutano husika ya ibada,
 - iv) wakati na mahali pa mikutano ya ibada,
 - v) kuchunguza ripoti kutoka kwa kamati, viongozi, mwekahazina, madarasa ya watoto, vikundi vya wanaume, wanawake, na vijana,
 - vi) kuwateua wachungaji na viongozi,
 - vii) kuteuliwa kwa wanawake na wanaume kuakilisha mikutano ya miezi mitatu, eneo na mwaka katika viwango vya juu,
 - viii) mapendekezo ya kusajiliwa kwa wanaume na wanawake ambao wameonyesha vipawa vyao vya huduma kwa watu na mkutano wa mwaka.
- f) Msimamizi mkuu:
- i) hufungua mkutano wa shughuli za kanisa kwa maombi,

- ii) ensures that all points of view are heard,
 - iii) offers statements that express the sense of the meeting, attempting to meet significant objections by offering modified versions of the statements, or proposing to postpone a decision to a later meeting if substantial unity is not reached.
- g) Making decisions:
- i) Statements receiving general approval are recorded in writing as official minutes.
 - ii) The presiding clerk is a servant of this process and does not advocate his or her own views.
 - iii) If, in rare cases, the presiding clerk feels that it is urgent to express his or her own opinion, he or she vacates the presiding clerk's chair and becomes an ordinary member for the consideration of that item of business. The assistant presiding clerk or the recording clerk assumes the clerk's role until that item of business has been completed.
- h) Other responsibilities of the presiding clerk:
- i) to receive correspondence directed to the monthly meeting, replying only upon instruction of the monthly meeting,
 - ii) to submit records and certify actions of the meeting, such as marriages or burials, to the civil authorities and to the yearly meeting,
 - iii) to ensure that the minutes and membership records are kept in a secure place, are up to date, and are available to anyone who wishes to see them.
- i) The presiding clerk has no other powers than those enumerated above. When the pastor is present, the presiding clerk does not officiate at meetings for worship.
 - j) The vice presiding clerk serves as presiding officer of the meeting for church governance in the absence of the presiding clerk.
 - k) The recording clerk: During the meeting for business, as the presiding clerk is discerning the will of the members, the recording

- ii) huhakikisha kuwa maoni ya wote yamesikizwa,
 - iii) hutoa maelezo yanayolenga kiini cha mkutano, akijaribu kuzingatia maoni tofauti kwa kutoa mapendekezo mengine ama kupendekeza kuhairisha mkutano ikiwa hakuna kuafikiana.
- g) Kufanya maamuzi:
- i) Taarifa zilizoafikiwa na wengi huandikwa kama kumbukumbu.
 - ii) Msimamizi mkuu ni mtumishi wa mchakato huu na hawezi kupendekeza wala kutoa maoni yake.
 - iii) Iwapo, na ni nadra, msimamizi mkuu atahisi kuwa ni lazima atoe maoni yake, itambidi aiache kazi ya uwenyekiti wa hicho kikao ili awe kama mwanachama mwingine na nafasi yake ichukuliwe na naibu wa msimamizi mkuu au mwandishi hadi mwisho wa kujadiliwa kwa hoja hiyo.
- h) Majukumu mengine ya msimamizi mkuu:
- i) kupokea barua za mkutano wa mwezi na akijibu tu anavyoelekezwa,
 - ii) kutoa taarifa na kuthibitisha maamuzi ya mkutano kama vile ndoa au mazishi kwa tawala za umma na mkutano wa mwaka,
 - iii) kuhakikisha kuwa kumbukumbu na rekodi zote ni sahihi na zimehifadhiwa vizuri kwa yeyote anayetaka kuziingalia.
- i) Msimamizi mkuu hana mamlaka mengine isipokuwa yale yaliyotajwa hapo awali. Mchungaji akiwepo, msimamizi mkuu haongozi mikutano ya ibada.
 - j) Naibu wa msimamizi mkuu huwa msimamizi mkuu mtendaji wa mkutano wa uongozi wa kanisa wakati msimamizi mkuu hayupo.
 - k) Karani mwandishi: Wakati wa mkutano rasmi, msimamizi mkuu anapotafakari juu ya nia ya wanachama, karani mwandishi husaidia

clerk assists by writing down the presiding clerks' suggested minutes, and makes a clear record of the minutes which are approved by the members.

l) Financial affairs:

- i) The village and monthly meeting maintains a bank account in the name of the monthly meeting, and appoints signing officers (presiding clerk, recording clerk and treasurer) who are authorised to make inquiries and withdrawals. At all times two signatures are required: the treasurer plus one of the clerks.
- ii) All bank records must be meticulously (carefully and accurately) preserved and made available to any associate or full member of the church or any officer of the yearly meeting who wishes to see them.
- iii) Every meeting is served by a treasurer and a vice treasurer. The treasurer should work with a finance committee and be audited.
- iv) Each meeting tithes 10% of its income. (Village meeting tithes to monthly meeting, monthly meeting to yearly meeting, and yearly meeting to Friends United Meeting.) Each member of the meeting should tithe his/her 10% income to the meeting, beginning from the village meeting.
- v) No treasurer or other church officer may make any withdrawal from the monthly meeting's bank account or write a cheque on the bank account's funds or make financial promises in the name of the monthly meeting except on the explicit instructions of the monthly meeting or a committee authorised by the monthly meeting to make such expenditures, or according to a schedule of regular payments authorised in advance by the monthly meeting or relevant committee.
- vi) The monthly meeting appoints auditors to conduct audits of the monthly meeting's accounts every two years or as requested by the monthly meeting. The yearly meeting may also require audits. Auditors may not be officers of the meeting or relatives

kwa kunakili yaliyopendekezwa na msimamizi mkuu kama kumbukumbu sahihi za yale yaliyothibitishwa na wanakamati.

l) Shughuli za fedha:

- i) Mikutano ya kijiji na ya mwezi huwa na akaunti ya benki kwa jina la mkutano wa mwezi, na huwateua viongozi (msimamizi mkuu, karani mwandishi, na mweka hazina) ambao huwa wameidhinishwa kushughulikia masuala ya fedha. Ni lazima watu wawili watie sahihi: mweka hazina na mmoja wao.
symbols, and ought ever to be received in the light of His own emphatic declaration, “The words that I speak unto you, they are spirit, and they are life” (John 6: 63). The old covenant was full of ceremonial symbols; the new covenant, to which our Savior alluded at the last supper, is expressly declared by the prophet to be “not according to the old” (Jeremiah 31:32; Hebrews 8:9). We cannot believe that in setting up this new covenant the Lord Jesus intended an institution out of harmony with the spirit of this prophecy. The eating of His body and the drinking of His blood cannot be an outward act. They truly partake of them who habitually rest upon the sufferings and death of our Lord as their only hope, and to whom the indwelling Spirit gives to drink of the fullness that is in Christ. It is this inward and spiritual partaking that is the true supper of the Lord.

The presence of Christ with His church is not designed to be by symbol or representation, but in the real communication of His own Spirit. “I will pray the Father, and he shall give you another Comforter, that he may abide with you forever” (John 14:16). Convincing of sin, testifying of Jesus, taking of the things of Christ, this blessed Comforter communicates to the believer and to the church, in a gracious, abiding manifestation the REAL PRESENCE of the Lord. As the great Remembrancer, through whom the promise is fulfilled, He needs no ritual or priestly intervention in bringing to the experience the true commemoration and communion. “Behold,” saith the risen Redeemer, “I stand at the door, and knock if any man hear my voice, and open the door, I will come in to him, and will sup with him, and he with me” (Revelation 3:20). In an especial manner, when assembled for congregational worship, are believers invited to the festival of the Savior’s peace, and, in a united act of faith and love, unfettered by any outward rite or ceremonial, to partake together of the body that was broken and of the blood that was shed for them, without the gates of Jerusalem. In such a worship they are enabled to understand the words of the apostle as expressive of a sweet and most real experience: “The cup of blessing which we bless, is it not the communion of the blood of Christ? The bread which we break, is it not the communion of the body of Christ? For we being many are one bread, and one body for we are all partakers of that one bread” (1 Corinthians 10:16, 17).

kuosha miguu ya mwenzake, yalikuwa katika mifano, na ni lazima yaeleweke katika mtazamo wa uzito wa maneno yake, “maneno haya niliyowaambia ni roho tena ni uzima” (Yohana 6:63). Agano la kale lilikuwa limejaa mifano mingi ya sherehe; agano jipya ambayo Mwokozi wetu ametaja katika karamu ya mwisho, imeelezwa wazi na nabii kuwa “agano hili halitakuwa kama lile lililofanya na baba zao” (Yeremia 31:32; Waebrania 8:9). Hatuwezi kuamini kwamba kwa kuanzisha hili agano jipya, Bwana Yesu alikusudia asasi tofauti na ukweli wa unabii huu. Kula mwili wake na kunywa kwa damu yake si kitendo cha nje. Wanaoshiriki kikamilifu katika vitendo hivi ni wale ambao kwa kawaida wanaamini mateso na kifo cha Bwana wetu kama tumaini lao la pekee na ambao Roho wao huwapa ukamilifu wa kuwa ndani ya Kristo. Ni huu ushirika wa kindani na wa kiroho ndio ukweli wa meza ya Bwana.

Uwepo wa Kristo na kanisa lake haijabuniwa kwa ishara wala kwa uwakilishi, lakini kwa mawasiliano halisi ya Roho wake. “Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine akae nanyi milele” (Yohana 14:16). Akisadikisha dhambi, kushuhudia Yesu, akishiriki kwa mambo ya Kristo, huyu Mfariji wa baraka huwasiliana na muumini na kanisa, kwa neema, inayodhihirisha wazi uhalisia wa kuwepo kwa Bwana. Kama kumbukumbu ambayo, kupitia kwake ahadi inatimilika, hahitaji sherehe wala mwingilio wa kikuhani kuleta tukio la kamili la ukumbusho na ushirika wa kweli. “Tazama,” asema Mkombozi aliyefufuka, “nasimama mlangoni nabisha. Kama mtu ye yote akisikia sauti yangu na kufungua mlango, nitaingia ndani na kula pamoja naye, naye pamoja nami” (Ufunuo 3:20). Katika hali ya kipekee, tunapokusanyika kwa ibada ya pamoja, waumini wote wamealikwa kwa karamu ya amani ya Mwokozi, na kwa njia ya umoja wa imani na upendo, usiyofungwa na kanuni za kawaida wala sherehe, kushiriki pamoja kwa mwili uliomegwa na damu iliyomwagika kwa ajili yao, nje ya milango ya Yerusalemi. Katika ibada kama hiyo wanawezeshwa kuelewa maneno ya mtume kama yanayoelezea tukio lililo tamu na halisi: “Je, kikombe cha baraka ambacho tunakibariki, si ushirika katika damu ya Kristo? Mkate tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo? Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja, kwa kuwa wote twashiriki mkate mmoja” (1 Wakorintho 10:16, 17).

Public Worship

Worship is the adoring response of the heart and mind to the influence of the Spirit of God. It stands neither in forms nor in the formal disuse of forms; it may be without words as well as with them, but it must be in spirit and in truth (John 4: 24). We recognize the value of silence, not as an end, but as a means toward the attainment of the end; a silence, not of listlessness or of vacant musing, but of holy expectation before the Lord. Having become His adopted children through faith in the Lord Jesus Christ, it is our privilege to meet together and unite in the worship of Almighty God, to wait upon Him for the renewal of our strength, for communion one with another, for the edification of believers in the exercise of various spiritual gifts, and for the declaration of the glad tidings of salvation to the unconverted who may gather with us. This worship depends not upon numbers. Where two or three are gathered together in the name of Christ there is a church, and Christ, the living Head, in the midst of them. Through His mediation, without the necessity for any inferior instrumentality, is the Father to be approached and reverently worshipped. The Lord Jesus has forever fulfilled and ended the typical and sacrificial worship under the law, by the offering up of Himself upon the cross for us, once for all. He has opened the door of access into the inner sanctuary, and graciously provided spiritual offerings for the service of His temple, suited to the several conditions of all who worship in spirit and in truth. The broken and the contrite heart, the confession of the soul prostrate before God, the prayer of the afflicted when he is overwhelmed, the earnest wrestling of the spirit, the outpouring of humble thanksgiving, the spiritual song and melody of the heart (Ephesians 5:19), the simple exercise of faith, the self-denying service of love, these are among the sacrifices which He, our merciful and faithful High Priest, is pleased to prepare, by His Spirit, in the hearts of them that receive Him, and to present with acceptance unto God.

By the immediate operations of the Holy Spirit, He, as the Head of the church, alone selects and qualifies those who are to present His messages or engage in other service for Him; and hence, we cannot commit any formal arrangement to any one in our regular meetings for worship. We are well aware that the Lord has provided a diversity of gifts (1 Corinthians 12:4-6) for the needs both of the church and of the world, and we desire that the

Ibada ya Pamoja

Ibada ni kiitikio cha moyo na akili kwa ushawishi wa Roho wa Mungu. Haitaji mipango wala haikatazi mipango; inaweza kuwa bila kuongea ama na kuongea, lakini lazima iwe katika roho na kweli (Yohana 4:24). Tunatambua umuhimu wa unyamavu, si kama kitu cha lazima bali kama njia ya kufikia lengo, unyamavu, usio wa utepetevu wala wa tafakari tupu, lakini wa matarajio matakatiifu mbele ya Bwana. Baada ya kufanywa watoto wake wateule kupitia kwa imani katika Bwana Yesu Kristo, ni faida kwetu kukutana pamoja na kuungana kwa kumuabudu Mungu Mkuu, kumuomba ili kupata nguvu zetu upya, kwa ushirika pamoja na wengine, kwa kufundisha waumini matumizi ya aina mbali mbali ya vipawa vya kiroho, na kwa tangazo la habari njema za wokovu kwa wasioamini ambao wanaweza kukusanyika pamoja nasi. Ibada hii haitegemei idadi. Mahali wawili au watatu wamekusanyika katika jina la Kristo ni kanisa, na Kristo, Kiongozi aishie, ni miongoni mwao. Kupitia kwa upatanishi wake, bila kuhitaji kiunganishi chochote, ni Baba wa kuabudiwa kwa utukufu. Bwana Yesu daima ametimiza na kumaliza ibada ya ishara na dhabihu chini ya sheria, kwa kujitoa mwenyewe msalabani kwa ajili yetu mara moja. Amefungua mlango wa kuingia mahali patakatiifu pakuu, na kwa neema ametoa vitu vya kiroho kwa huduma ya kanisa lake, kulingana na hali zote za wale wanaomuabudu. Moyo myenyekevu na uliovunjika, ungamo la nafsi nyenyekevu mbele ya Mungu, maombi ya mwenye kuteseka akiwa amezidiwa, juhudi za dhata za kiroho, wingi wa shukrani zenye unyenyekevu, wimbo wa kiroho na sauti ya moyo (Waefeso 5:19), zoezi rahisi la imani, utumishi wa kujitolea wa upendo, ni baadhi ya dhabihu, Kuhani Mkuu, mwenye huruma na imani amependezwa kutayarisha, kwa Roho yake, katika mioyo ya wale waliomkubali, na kumkabidhi Mungu.

Kwa matendo ya moja kwa moja ya Roho Mtakatifu, yeye kama Kiongozi wa kanisa, huwateua wale awapao ujumbe wake ama kuwashirikisha katika huduma nyingine yake; na kwa hivyo hatuwezi kukabidhi mpangilio mwingine rasmi kwa yeyote katika mikutano yetu ya mara kwa mara ya kuabudu. Tunafahamu vizuri kuwa Bwana ametoa vipawa mbali mbali (1 Wakorintho 12:4-6) kwa mahitaji ya kanisa na ya ulimwengu, na

church may feel her responsibility, under the government of her Great Head, in doing her part to foster these gifts, and in making arrangements for their proper exercise.

It is not for individual exaltation, but for mutual profit, that the gifts are bestowed (1 Corinthians 12:7); and every living church, abiding under the government of Christ, is humbly and thankfully to receive and exercise them in subjection to her Holy Head. The church that quenches the Spirit and lives to itself alone must die.

We believe the preaching of the Gospel to be one of the chief means, divinely appointed, for the spreading of the glad tidings of life and salvation through our crucified Redeemer, for the awakening and conversion of sinners, and for the comfort and edification of believers. As it is the prerogative of the Great Head of the church alone to select and call the ministers of His Gospel, so we believe that both the gift and the qualification to exercise it must be derived immediately from Him, and that, as in the primitive church, so now also, He confers spiritual gifts upon women as well as upon men, agreeably to the prophecy recited by the Apostle Peter, "It shall come to pass in the last days, saith God, I will pour out of my Spirit upon all flesh and your sons and your daughters shall prophesy" (Acts 2:17), respecting which the apostle declares, "The promise is unto you, and to your children, and to all that are afar off, even as many as the Lord our God shall call" (Acts 2:39). As the gift is freely received so it is to be freely exercised (Matthew 10:8; see also Acts 20:33-35), in simple obedience to the will of God.

Spiritual gifts, precious as they are, must not be mistaken for grace; they add to our responsibility, but do not raise the minister above his brethren or sisters. They must be exercised in continued dependence upon our Lord, and blessed is that ministry in which man is humbled, and Christ and His grace exalted. "He that is greatest among you," said our Lord and Master, "let him be as the younger; and he that is chief, as he that doth serve I am among you as he that serveth" (Luke 22:26, 27).

While the church cannot confer spiritual gifts, it is its duty to recognize and foster them, and to promote their efficiency by all the means in its power. And while, on the one hand, the Gospel should never be preached for

tunatumaini kuwa kanisa litawajibika, chini ya uongozi wa Kiongozi wake Mkuu, katika kutekeleza wajibu wake, kuviboresha vipaji hivi kwa mipangilio ya matumizi bora.

Si kwa kumtukuza mwanadamu binafsi bali kwa manufaa ya wote, ndiposa hivi vipawa vinapeanwa (1 Wakorintho 12:7); na kila kanisa linalotii mamlaka ya Kristo linapokea kwa unyenyekevu na utiifu kwa ajili ya Uongozi wake Mtakatifu. Kanisa linalozimisha Roho na kuishi kivyake lazima liangamie.

Tunaamini kuhubiri injili kama njia mojawapo muhimu ya kueneza habari njema ya uzima na wokovu kupitia kwa Mkombozi aliyesulubiwa, kwa kuzindua na kubadilisha mwenye dhambi, na kwa kuwafaraji na kuwafundisha waumini. Kama ulivyo uwezo wa Kiongozi Mkuu wa kanisa wa kuwateua watumishi wa injili yake, ndivyo tunavyoamini kwamba kipawa na uwezo wa kutenda lazima utoke kwake, na kwamba kama ilivyokuwa katika kanisa la kale, ni vivyo hivyo hata sasa, huwapatia vipawa vya kiroho kwa wanawake na wanaume kulingana na unabii kama ulivyokaririwa na Mtume Petro, "katika siku za mwisho, asema Bwana, nitamimina Roho wangu juu ya wote wenye mwili. Wana wenu na binti zetu watatabiri" (Matendo 2:17), na kwa kuzingatia hili mtume anasema "kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili uenu na watoto wenu na kwa kale wote walio mbali na kila mtu ambaye Bwana Mungu wetu atamwita amjie" (Matendo 2:39). Kama vile kipawa kinavyopokelewa bure na vivyo hivyo ndivyo kinapaswa kitumiwe (Mathayo 10:8; tazama pia Matendo 20:33-35), kwa utiifu rahisi wa mapenzi ya Mungu.

Vipawa vya kiroho, muhimu jinsi vilivyo, visichukuliwe kama neema; ni sehemu ya majukumu yetu, lakini havimuini mhuduma akawa juu ya ndugu au dada zake. Lazima vitumike kwa kumtegemea Bwana wetu, na imebarikiwa ile huduma ambayo mwanadamu amejinyenyekeza, na Kristo na neema yake kuinuliwa. "Yeye aliye mkuu kuliko wote miongoni mwenu," akasema Bwana wetu "inampasa kuwa kama yeye aliye mdogo wa wote, naye atawalaye na awe kama yeye ahudumuye Mimi niko miongoni mwenu kama yule ahudumiaye" (Luka 22:26, 27).

Hata kama kanisa haliwezi kupeana vipawa, ni wajibu wake kuvitambua na kuvikuzua, na kwa uwezo wake wote, ili kuviwezesha kutoa huduma bora. Kwa upande mmoja, injili isihubiriwe kwa sababu ya pesa, (Matendo 8:20;

money (Acts 8:20; 20:33-35), on the other, it is the duty of the church to make such provision that it shall never be hindered for want of it.

The church, if true to her allegiance, cannot forget her part in the command, "Go ye into all the world, and preach the gospel to every creature" (Mark 16:15). Knowing that it is the Spirit of God that can alone prepare and qualify the instruments who fulfill this command, the true disciple will be found still sitting at the feet of Jesus, listening that he may learn, and learning that he may obey. He humbly places himself at his Lord's disposal, and, when he hears the call, "Whom shall I send, and who will go for us?" is prepared to respond, in childlike reverence and love, "Here am I; send me" (Isaiah 6:8).

Prayer and Praise

Prayer is the outcome of our sense of need, and of our continual dependence upon God. He who uttered the invitation, "Ask, and it shall be given you" (Matthew 7:7), is Himself the Mediator and High Priest who, by His Spirit, prompts the petition, and who presents it with acceptance before God. With such an invitation, prayer becomes the duty and the privilege of all who are called by His name. Prayer is, in the awakened soul, the utterance of the cry, "God be merciful to me a sinner" (Luke 18:13), and, at every stage of the believer's course, prayer is essential to his spiritual life. A life without prayer is a life practically without God. The Christian's life is a continual asking. The thirst that prompts the petition produces, as it is satisfied, still deeper longings, which prepare for yet more bounteous supplies, from Him who delights to bless. Prayer is not confined to the closet. When uttered in response to the promptings of the Holy Spirit, it becomes an important part of public worship, and, whenever the Lord's people meet together in His name, it is their privilege to wait upon Him for the spirit of grace and supplications (Zechariah 12:10). A life of prayer cannot be other than a life of praise. As the peace of Christ reigns in the church, her living members accept all that they receive as from His pure bounty, and each day brings them fresh pledges of their Father's love. Satisfied with the goodness of His house, whether as individuals, in families, or in congregations, they will be still praising Him (Psalm 84:4), heart answering to heart, "Bless the Lord, O my soul and all that is within me, bless his holy name" (Psalm 103:1).

20:33-35), na kwa upande mwingine, jukumu la kanisa kutoa pesa ili kazi ya kueneza injili isikwame.

Kanisa, likiwa kweli kwa utiifu wake, haliwezi kusahau jukumu lake katika amri, "enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe" (Marko 16:15). Mkijua kwamba ni Roho wa Mungu pekee ambaye anaweza kuandaa na kuwezesha wanadamu kutimiza amri hii, mwanfunzi wa kweli atapatikana ameketi chini ya miguu ya Yesu, akisikiza ili ajifunze na kujifunza ili kutii. Kwa unyenyekevu anajiweka mbele ya Bwana, na anaposikia mwito, "nimtume nani? Ni nani atakayekwenda?" yuko tayari kuitikia, kwa heshima kuu na upendo kama wa kitoto, "mimi hapa. Nitume mimi!" (Isaya 6:8)

Maombi na Sifa

Maombi ni matokeo ya hitaji, na kuendelea kwetu kumtegemea Mungu. Yeye aliyetoa mwaliko, "ombeni nanyi mtapewa" (Mathayo 7:7), ni mwenyewe Mpatanishi na Kuhani Mkuu ambaye, kwa Roho yake, huchochea maombi, na huyawazilisha yakakubalika mbele ya Mungu. Kwa mwaliko kama huu, huwa jukumu na faida kwa wale wote walioitwa kwa jina lake. Maombi ni, katika nafsi iliyosisimuliwa, tamko la kilio, "Mungu, nihurumie mimi mwenye dhambi" (Luka 18:13), na katika kila hatua ya maisha ya muumini, maombi ni muhimu kwa maisha yake ya kiroho. Kwa hakika, maisha bila maombi ni maisha bila Mungu. Maisha ya mkristo ni ya maombi kila mara. Hamu inayoleta maombi husababisha, ikiridhika, hamu zaidi ambayo humtayarisha kupokea zaidi kutoka kwa yule ambaye hufurahia kubariki. Maombi hayajafungiwa tu faraghani. Yakitamkwa kwa kuitikia msukumo wa Roho Mtakatifu, huwa sehemu muhimu ya ibada ya pamoja, na wakati wanadamu wa Mungu wanapokutana pamoja katika jina lake, ni faida yao kumwomba kwa roho ya neema na usaidizi kutoka kwa Mungu (Zekaria 12:10). Maisha ya maombi hayawezi kuwa maisha bila sifa. Kama vile amani ya Kristo inavyotawala kanisa, wafuasi wake hukubali yote wanayopokea kutoka kwa wingi wake, na kila siku huwaletea ahadi nzuri za upendo wa Baba yao. Wakiridhishwa na uzuri wa nyumba yake, wakiwa pekee yao au kama jamaa, ama katika mikusanyiko, watakuwa wangali wanamsifu (Zaburi 84:4), moyo ukijibu moyo, "ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, vyote vilivyomo ndani yangu vilihimidi jina lake takatifu" (Zaburi 103:1).

Liberty of Conscience in its Relation to Civil Government

That conscience should be free, and that in matters of religious doctrine and worship man is accountable only to God, are truths which are plainly declared in the New Testament; and which are confirmed by the whole scope of the Gospel, and by the example of our Lord and His disciples. To rule over the conscience, and to command the spiritual allegiance of His creature man, is the high and sacred prerogative of God alone. In religion every act ought to be free. A forced worship is plainly a contradiction in terms, under that dispensation in which the worship of the Father must be in spirit and in truth (John 4:24).

We have ever maintained that it is the duty of Christians to obey the enactments of civil government, except those which interfere with our allegiance to God. We owe much to its blessings. Through it we enjoy liberty and protection, in connection with law and order. Civil government is a divine ordinance (Romans 13:1; 1 Peter 2:13-16), instituted to promote the best welfare of man, hence magistrates are to be regarded as God's ministers who should be a terror to evil doers and a praise to them that do well. Therefore, it is with us a matter of conscience to render them respect and obedience in the exercise of their proper functions.

Marriage

Marriage is an institution graciously ordained by the Creator Himself, for the help and continuance of the human family. It is not a mere civil contract, and ought never to be entered upon without a reference to the sanction and blessing of Him who ordained it. It is a solemn engagement for the term of life (Matthew 19:5, 6), designed for the mutual assistance and comfort of both sexes, that they may be help-meets to each other in things temporal and spiritual. To this end it should imply concurrence in spiritual as well as temporal concerns, and should be entered upon discreetly, soberly, and in the fear of the Lord.

Peace

We feel bound explicitly to avow our unshaken persuasion that all war is utterly incompatible with the plain precepts of our divine Lord and Law-giver, and the whole spirit of His Gospel, and that no plea of necessity or policy, however urgent or peculiar, can avail to release either individuals or

Uhuru wa Dhamiri na Uhusiano wake na Serikali ya Raia

Dhamiri inafaa kuwa huru, na katika mafundisho ya kidini na ibada, mwanadamu anawajibika tu kwa Mungu, ni ukweli uliotangazwa wazi katika agano jipya; na umethibitishwa na injili yote kwa jumla, na kwa mfano wa Bwana wetu na wanafunzi wake. Kutawala dhamiri na kuamuru utiifu wa kiroho wa mwanadamu, ni jukumu takatifu la Mungu pekee. Katika dini kila tendo lazima liwe huru. Ibada ya kulazimishwa ni kinyume, chini ya mpango ya Mungu ambao ibada ya Baba lazima iwe kwa roho na kweli (Yohana 4:24).

Tumeshikilia kwamba ni jukumu la kila mkristo kutii sheria za serikali ya raia, isipokuwa zile zinazopinga uaminifu wetu kwa Mungu. Tuna shukrani kwa baraka za serikali ya raia. Kupitia kwake tunafurahia uhuru na ulinzi, kutokana na sheria na utulivu. Serikali ya raia ni agizo takatifu (Waroma 13:1; 1 Petro 2:13-16), ilianzishwa kuendeleza maslahi bora ya mwanadamu, kwa hivyo mahakimu wanafaa kuchukuliwa kama watumishi wa Mungu ambao ni tisho kwa waovu na sifa ni kwa wale watendao mema. Kwa hivyo, kwetu ni jambo la dhamiri kuwapa heshima na kuwatii katika utendaji wa majukumu yao halali.

Ndoa

Ndoa ni asasi iliyoanzishwa kwa neema ya Muumba mwenyewe, kwa uendelezaji wa kizazi cha mwanadamu. Sio tu mkataba wa kwaida wa binadamu, na lazima ufanywe kwa idhini na baraka ya yule aliyeamuru. Ni upatanishi takatifu wa maisha (Mathayo 19:5, 6), kwa nia ya usaidizi na utulivu wa jinsia zote, ili wawe wakisaidiana kwa maisha ya kawaida na ya kiroho. Kwa hivyo hii ina maana kuwa ni mapatano ya mambo ya kiroho pamoja na ya kawaida, na ianzishwe kwa uangalifu, fikira pevu na utiifu kwa Mungu.

Amani

Tunajihusisha na ushawishi usiopingika kwamba vita vyote haviambatani kabisa na kanuni wazi za Bwana wetu mtakatifu, mwasisi wa sheria, na kusudi kuu la injili yake, na kuwa hakuna ombi la lazima wala sera ikiwa ya dharura au pekee ambayo inaweza kuwafanya wanadamu au mataifa yasiitii

nations from the paramount allegiance which they owe to Him who hath said, "Love your enemies" (Matthew 5:44; Luke 6:27). In enjoining this love, and the forgiveness of injuries, He who has bought us to Himself has not prescribed for man precepts which are incapable of being carried into practice, or of which the practice is to be postponed until all shall be persuaded to act upon them. We cannot doubt that they are incumbent now, and that we have in the prophetic Scriptures the distinct intimation of their direct application not only to individuals, but to nations also (Isaiah 2:4, Micah 4:1). When nations conform their laws to this divine teaching, wars must necessarily cease.

We would, in humility, but in faithfulness to our Lord, express our firm persuasion that all the exigencies of civil government and social order may be met under the banner of the Prince of Peace, in strict conformity with His commands.

Oaths

We hold it to be the inalienable privilege of the disciple of the Lord Jesus that his statements concerning matters of fact within his knowledge should be accepted, under all circumstances, as expressing his belief as to the fact asserted. We rest upon the plain command of our Lord and Master, "swear not at all" (Matthew 5:34); and we believe any departure from this standard to be prejudicial to the cause of truth and to that confidence between man and man, the maintenance of which is indispensable to our mutual well being. This command, in our persuasion, applies not to profane swearing only, but to judicial oaths also. It abrogates any previous permission to the contrary, and is, for the Christian, absolutely conclusive.

The First Day of the Week

Whilst the remembrance of our Creator ought to be at all times present with the Christian, we would express our thankfulness to our Heavenly Father that He has been pleased to honor the setting apart of one day in seven for the purpose of holy rest, religious duties, and public worship; and we desire that all under our name may avail themselves of this great privilege as those who are called to be risen with Christ, and to seek those things that are above where He sitteth at the right hand of God (Colossians 3:1). May the release thus granted from other occupations be diligently improved. On this day of the week especially ought the households of

yale muhimu ambayo kwayo kuna utiifu mkumbwa kwake kama anavyosema mwenyewe, "wapendeni adui zenu" (Mathayo 5:44; Luka 6:27). Kwa kuamuru upendo huu na msamaha wa maumivu, yule aliyetuleta kwake hawezi kumpatia mwanadamu maagizo ambayo hayawezi kutekelezwa, au kuhahirishwa hadi wote washawishike kuyatekeleza. Hatuna shaka kwamba ni muhimu sasa, katika maandiko ya kinabii kuna ushawishi wa utekelezaji wake si kwa wanadamu tu bali hata kwa mataifa (Isaya 2:4, Mika 4:1). Wakati mataifa yanasawasisha sheria zao kwa fundisho hili takatifu, vita havina budi kukoma.

Kwa unyenyekevu na uaminifu kwa Bwana wetu, tunatoa ushawishi wetu thabiti kwamba mambo yote ya serikali ya raia na utulivu wa kijamii yawe chini ya nembo ya Mfalme wa Amani kuambatana na amri zake.

Viapo

Tunaamini kuwa faida isiyoondolewa ya mwanafunzi wa Bwana Yesu kuwa taarifa zake kuhusu mambo yake ya hakika katika fahamu yake yanakubalika, kwa vyovyote vile, kama imani yake kwa jambo hakika alilosema. Tunaamini amri dhahiri ya Bwana wetu, "msiape kabisa" (Mathayo 5:34); na tunaamini kukiuka kanuni hii ni kwenda kinyume na ukweli na uaminifu kati ya mwanadamu na mwenzake, utunzi wake ni kitu ambacho ni lazima kwa manufaa yao wote wawili. Kwa ushawishi wetu, amri hii haiathiri tu kuapa kwa maneno machafu, lakini hata kwa viapo vya mahakamani. Inabililisha ruhusa yeyote ya awali na ni thibidisho la kuondoa shaka kwa mkristo.

Siku ya Kwanza ya Wiki

Ingawa kumkumbuka Muumba wetu kunafaa kuwa kwa wakati wote kwa mkristo, tunatoa shukrani zetu kwa Baba wetu wa Mbinguni kwamba amependezwa kutenga siku moja kati ya saba kwa madhumuni ya mapumziko matakatifu, majukumu ya kidini, na ibada ya pamoja; tunatamani kwamba wote kwa jina letu wajitokeze na kuchukua faida hii kuu kama wale walioitwa kufufuka pamoja na Kristo, na kutafuta vitu vilivyoo juu ambapo ameketi katika mkono wa kuume wa Mungu (Wakolosai 3:1). Na kufunguliwa huku kutoka kwa kazi zingine kuhimarishwe kabisa. Katika siku hii ya wiki, inapasa jamii na Marafiki kukusanyika na kusoma maandiko

Friends to be assembled for the reading of the Scriptures and for waiting upon the Lord; and we trust that, in a Christianly wise economy of our time and strength, the engagements of the day may be so ordered as not to frustrate the gracious provision thus made for us by our Heavenly Father, or to shut out the opportunity either for public worship or for private retirement and devotional reading.

In presenting this declaration of our Christian faith, we desire that all our members may be afresh encouraged, in humility and devotedness, to renewed faithfulness in fulfilling their part in the great mission of the church, and through the church to the world around us, in the name of our crucified Redeemer. Life from Christ, life in Christ, must ever be the basis of life for Christ. For this we have been created and redeemed, and by this alone can the longings of our immortal souls be satisfied.

na kumngojea Bwana; na tunaamini kwamba, katika hali ya kikristo, ya matumizi mazuri ya wakati wetu na nguvu, kazi za siku zinaweza kupangwa vizuri na kwa neema ili zisiharibu kile alichotupatia Baba wetu wa Mbinguni, wala kufungia nje nafasi ya ibada ya pamoja au usomaji wa kumuabudu Mungu faraghani.

Kwa kuanzisha tangazo hili la imani ya ukristo wetu, tunatamani kwamba wafuasi wetu wote waweze kutiwa moyo, kwa unyenyekevu na uaminifu, kwa uaminifu mpya katika kutimiliza sehemu yao katika huduma kuu ya kanisa na kupitia kwa kanisa kwa ulimwengu, katika jina la Mkombozi wetu aliyesulubiwa. Uzima kutoka kwa Kristo, uzima ndani ya Kristo, daima uwe msingi wa maisha katika Kristo. Kwa haya tumeumbwa na kukombolewa, na kwa haya pekee ndiyo hamu ya kudumu milele ya nafsi zetu zinaweza kuridhishwa.

Appendix B – Historical Statements of Faith:

Extracts from George Fox's letter to the Governor of Barbados, 1671

We own and believe in the only wise, omnipotent, and everlasting God, the Creator of all things both in heaven and earth, and the Preserver of all that He hath made; who is God over all, blessed forever; to whom be all honor, glory, dominion, praise, and thanksgiving, both now and for evermore.

And we own and believe in Jesus Christ, His beloved and only begotten Son, in whom He is well pleased; who was conceived by the Holy Ghost, and born of the Virgin Mary; in whom we have redemption through His blood, even the forgiveness of sins; who is the express image of the invisible God, the first-born of every creature, by whom were all things created that are in heaven and in earth, visible and invisible, whether they be thrones, dominions, principalities, or powers; all things were created by Him. And we own and believe that He was made a sacrifice for sin, who knew no sin, neither was guile found in His mouth; that He was crucified for us in the flesh, without the gates of Jerusalem; and that He was buried, and rose again the third day by the power of His Father, for our justification; and that He ascended up into heaven, and now sitteth at the right hand of God. This Jesus, who was the foundation of the holy prophets and apostles, is our foundation; and we believe that there is no other foundation to be laid but that which is laid, even Christ Jesus; who tasted death for every man, who shed His blood for all men, is the propitiation for our sins, and not for ours only, but also for the sins of the whole world according as John the Baptist testified of Him when he said, "Behold the Lamb of God, that taketh away the sin of the world!" (John 1:29) We believe that He alone is our Redeemer and Saviour, the Captain of our salvation who saves us from sin, as well as from hell and the wrath to come, and destroys the devil and his works; He is the Seed of the woman that bruises the serpent's head, to wit, Christ Jesus, the Alpha and Omega, the First and the Last. He is (as the Scriptures of truth

Nyongeza B – Masimulizi ya Kihistoria ya Imani:

Dondoo kutoka kwa Barua ya George Fox kwa Mtawala Wa Babadosi, 1671

Tunamjua na kuamini yule wa pekee wa hekima, mwenye enzi, na Mungu wa milele, Muumba wa vitu vyote mbinguni na duniani, na Mhifadhi wa vyote alivyoviumba; aliye Mungu juu ya vyote, aliyebarikiwa milele; kwake heshima yote, utukufu, ufalme, sifa, na shukrani, sasa na hata milele.

Na tunamjua na kuamini Yesu Kristo, Mwanawe mpendwa wa pekee, anayempendeza; ambaye mama yake alipata mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, na akazaliwa na Bikira Maria; ambaye ndani mwake tumepata ukombozi kwa damu yake, hata msamaha wa dhambi; aliye mfano kamili wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa kila kiumbe, kwa yeye vitu vyote vilivyoko mbinguni na juu ya nchi viliumbwa, vile vitu vinavyoonekana na vile visivyonekana, kama ni viti vya enzi, falme, wenye mamlaka au watawala, vitu vyote viliumbwa na yeye. Na tunajua na kuamini kwamba alifanywa kuwa dhabihu kwa dhambi, asiyetenda dhambi, wala hapakuwa na ujanja kinywani mwake; kwamba alisulubiwa katika mwili kwa niaba yetu, nje ya milango ya Yerusalemi; na kwamba alizikwa, na akafufuka tena siku ya tatu kwa uwezo wa Baba yake, kwa kuhesabiwa haki kwetu; na kwamba alipaa juu mbinguni, na sasa ameketi kwa mkono wa kuume wa Mungu. Huyu Yesu, aliyekuwa msingi wa manabii watakatifu na mitume ndiye msingi wetu, na tunaamini kwamba hakuna msingi mwingine utakaowekwa isipokuwa ule uliyokwisha wekwa, hata Kristo Yesu; aliyekufa kwa ajili ya kila mwanadamu, aliyemwaga damu yake kwa ajili ya wanadamu wote, ndiye kipatanisho cha dhambi zetu, na si zetu tu, lakini pia kwa dhambi za ulimwengu wote kama vile Yohana Mbatizaji alivyoshuhudia kwake aliposema, "tazama, Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" (Yohana 1:29) Tunaamini kuwa yeye pekee ndiye Mkombozi na Mwokozi wetu, Nahodha wa wokovu wetu atuokoaye kutoka kwa dhambi, na pia kutoka jehanamu na ghadhabu itakayokuja, na kuharibu

say of Him) our wisdom, righteousness, justification, and redemption; neither is there salvation in any other, for there is no other name under heaven given among men, whereby we may be saved. He alone is the Shepherd and Bishop of our souls; He is our Prophet, whom Moses long since testified of, saying, "A prophet shall the Lord your God raise up unto you of your brethren, like unto me; him shall ye hear in all things whatsoever he shall say unto you; and it shall come to pass, that every soul that will not hear that prophet shall be destroyed from among the people." (Acts 3:22-23)

He is now come in Spirit "and hath given us an understanding, that we may know him that is true." He rules in our hearts by His law of love and of life, and makes us free from the law of sin and death. We have no life, but of Him; for He is the quickening Spirit, the second Adam, the Lord from heaven, by whose blood we are cleansed, and our consciences sprinkled from dead works, to serve the living God. He is our Mediator, who makes peace and reconciliation between God offended and us offending; He being the Oath of God, the new covenant of light, life, grace, and peace, the author and finisher of our faith. This Lord Jesus Christ, the heavenly man, the Emmanuel, God with us, we all own and believe in; He whom the high-priest raged against, and said He had spoken blasphemy; whom the priests and elders of the Jews took counsel together against, and put to death; the same whom Judas betrayed for thirty pieces of silver, which the priests gave him as a reward for his treason; who also gave large money to the soldiers to broach a horrible lie, namely, "That his disciples came and stole him away by night while they slept." After He was arisen from the dead, the history of the Acts of the Apostles sets forth how the chief priests and elders persecuted the disciples of this Jesus, for preaching Christ and His resurrection. This, we say, is that Lord Jesus Christ, whom we own to be our life and salvation.

Concerning the Holy Scriptures, we believe that they were given forth by the Holy Spirit of God, through the holy men of God, who (as the Scripture itself declares, 2 Peter 1:21) "spake as they were moved by the Holy Ghost." We believe they are to be read, believed, and fulfilled (He that fulfills them is

Shetani na kazi zake; ni zao la mwanamke ambalo hugaribu kichwa cha nyoka, ni Kristo Yesu, mwanzo na mwisho. Yeye ni (kama maandiko ya kweli yanavyosema kumhusu) hekima yetu, uongofu, kuhesabiwa haki na ukombozi; hakuna wokovu katika mwingine, kwa kuwa hakuna jina jingine lilopewa wanadamu chini ya mbingu ili tuokoke. Yeye pekee ndiye Mchungaji na Askofu wa nafsi zetu; yeye ndiye Nabii wetu, ambaye Musa alishuhudia zamani, akisema "Bwana Mungu wenu atawainulia nabii kama mimi kutoka miongoni mwa ndugu zenu, itawapasa kumtii huyo kwa kila jambo atakalowaambia. Mtu ye yote ambaye hatamsikiliza huyo nabii, atakataliwa mbali kabisa na watu wake" (Matendo 3:22-23).

Amekuja kwa Roho "na ametupatia ufahamu, ili tumjue yeye kuwa kweli." Anatuongoza katika mioyo yetu kwa sheria ya upendo na uzima, na kutuweka huru kutoka kwa sheria ya dhambi na kifo. Hatuna uzima, isipokuwa wake; yeye ndiye Roho anayefufua, Adamu wa pili, Bwana kutoka mbinguni, ambaye kupitia kwa damu yake tumesafishwa, na nafsi zetu zimefufuliwa kutoka kwa kazi zilizokufa, kumtumikia Mungu aishiye. Yeye ndiye Mpatanishi wetu, atuleteaye amani na maridhiano kati ya Mungu aliyekosewa nasi wakosaji; yeye ndiye Ahadi ya Mungu, agano jipya la huru, uzima, neema na amani, muumba na thibitisho la imani yetu. Huyu Bwana Yesu Kristo, mwanadamu wa mbinguni, Imanueli, Mungu pamoja nasi, tunayemjua na kumuamini; yeye ambaye kuhani mkuu alimkasirikia, na kusema alikuwa amesema ukafiri; yeye ambaye makuhani na wazee wa Wayahudi walishauriana kumpinga, na kumuua; ni yeye yule Yuda alisaliti kwa vipande thelathini vya fedha, ambavyo makuhani walimpatia kama zawadi kwa uhaini wake; vile vile walitoa pesa nyingi kwa askari kuanzisha uongo mbaya, usemao "kuwa wanafunzi wake walikuja na kumuiba usiku walipokuwa wamelala." Alipofufuliwa kutoka kwa wafu, historia ya matendo ya mitume inatuonyesha jinsi makuhani wakuu na wazee walidhulumu wanafunzi wa Yesu, kwa kosa la kuhubiri Kristo na kufufuka kwake. Kwa hivyo, tunasema, ni huyo Bwana Yesu Kristo, ambaye tunamjua kuwa uzima na wokovu wetu.

Kuhusu maandiko matakatifu, tunaamini kuwa yaliletwa na Roho Mtakatifu wa Mungu, kupitia kwa wanadamu watakatifu wa Mungu, ambao (kama vile Biblia yenywe inavyosema, 2 Petro 1:21) "walinena yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na Roho Mtakatifu." Tunaamini yafaa kusomwa, kuaminika,

Christ); and they are “profitable for doctrine, for reproof, for correction, for instruction in righteousness, that the man of God may be perfect, thoroughly furnished unto all good works,” and “are able to make wise unto salvation through faith in Christ Jesus.” (2 Timothy 3:15-17)

– From the *Autobiography of George Fox*, edited by Henry Stanley Newman

na kutimizwa (yule ayatimizaye ni Kristo); na kuwa “lafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kuwaongoza na kuwafundisha katika haki ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila kazi njema” na “yanaweza kukuhekimisha upate wokovu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu” (2 Timotheo 3:15-17).

– Kutoka kwa *Tawasifu ya George Fox*, imehaririwa na Henry Stanley Newman